# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 013 JANUARI 2022




1. UTABIRI WA TMA NI WA UHAKIKA

2. UMOJA WA TAASISI ZA HALI YA HEWA ZA NCHI ZA SADC ZA AZIMIA UHUISHAJI WA SHUGHULI ZA UMOJA HUO



3. FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2022



JARIDA LA MWEZI



TOLEO NA. 013 JANUARI 2022

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

## KITAIFA

# UTABIRI WA TMA NI WA UHAKIKA

**Dar es Salaam**




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (MB) ametoa rai kwa watanzania kutumia vizuri taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kuwa taarifa hizo ni za uhakika. Mhe. Mwakibete, alizungumza hayo wakati wa ziara ya kutembelea Makao Makuu ya TMA, Ubungo Plaza, Tarehe 28/01/2022.

“kwa niaba ya Serikali na watanzania wengine na mimi binafsi, na kwa niaba ya waziri wangu mwenye kubeba dhamana ya wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Prof. Mbarawa, niwapongeze sana kwani taarifa zenu zimekuwa za uhakika na ni za kweli”. Alisema. Mhe. Mwakibete.

“Ni rai yangu kwa taasisi zingine na wizara zingine tutumie kikamilifu taarifa zinazotoka Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini, kwa namna hiyo tutakuwa tunaokoa hasara zilizo mbele yetu na kujipanga”. Aliongezea Mhe. Mwakibete.

Akizungumzia suala la changamoto ya maslahi duni, mhe. Waziri alisema kuwa atalisimamia suala hilo kwa kumshirikisha waziri mwenye dhamana na Mamlaka zingine ili kuona namna gani litashughulikiwa ili kuhakikisha wataalamu bingwa wa TMA hawahamia taasisi nyingine.

Katika hatua nyingine, Mhe. Mwakibete alisema, Serikali inatambua umuhimu wa TMA nchini, hivyo Mhe. Rais. Samia Suluhu Hassan kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha, ametenga jumla ya Tsh. Bil. 30 ili kukamilisha mtandao wa rada saba nchini.


Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Dkt. Buruhani Nyenzi alisema Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ni taasisi ya Muungano iliyoanzishwa kwa sheria Na. 2 ya mwaka 2019 ikifanya kazi zake Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar chini ya usimamizi wa Bodi ya TMA (Governing Board).

"Bodi ina jumla ya wajumbe 8, Mwenyekiti na Makamu ni wateule wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Mwenyekiti anatokea Tanzania Bara na Makamu wake anatokea Tanzania Zanzibar, Wajumbe wengine watano (5) wa Bodi ni wateule wa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya hali ya hewa ambapo Katibu wa Bodi hiyo ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka. Hawa wajumbe wanawakilisha sekta muhimu zinazotumia taarifa za hali ya hewa". Alisema Dkt. Nyenzi.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Agnes Kijazi ambaye pia ni Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), alifafanua kuwa Mamlaka imejiwekea malengo yanayolenga kutoa huduma bora zaidi na mahsusi kwa wadau na jamii ili kuchangia katika kutoa maamuzi na hatimaye kuleta maendeleo endelevu.

"Katika kutimiza azma ya Mhe. Rais ya kuwatumikia Watanzania na kutekeleza mipango ya Nchi yetu na ile ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ya utoaji wa huduma bora za hali ya hewa nchini, Mamlaka imejipanga kuboresha huduma za hali ya hewa na kuendelea kuboresha miundombinu ya hali ya hewa hapa nchini. Aidha mafunzo kwa wafanyakazi na uboreshaji wa mifumo ya menejimenti ya rasilimali fedha itaboreshwa zaidi. Katika kuongeza ubora wa huduma za hali ya hewa, Mamlaka imejiwekea malengo ya kushiriki na kuchangia katika shughuli za hali ya hewa za kitaifa, kikanda na kimataifa hususani katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO)". Alieleza Dkt. Kijazi.

Dkt. Kijazi aliishukuru serikali kwa kuendelea kuiwezesha Mamlaka kuwa na vitendea kazi vya kisasa na wataalamu wenye ujuzi ikiwa ni pamoja na kuipatia TMA Rada nyingine mbili ambazo ukamilikaji wake utapelekea kufikiwa kwa malengo ya muda mrefu ya kuwa na Rada 7 za hali ya hewa kwa nchi nzima.



KIMATAIFA

# UMOJA WA TAASISI ZA HALI YA HEWA ZA NCHI ZA SADC ZA AZIMIA UHUISHAJI WA SHUGHULI ZA UMOJA HUO

**Dar es Salaam**




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi akifungua kikao cha kwanza cha Bodi ya Umoja wa Taasisi za Hali ya Hewa za nchi za SADC "Meteorological Association of Southern Africa (MASA)" cha mwaka 2022 alipoongoza kikao hicho kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 26 Januari, 2022. Kushoto kwake ni Meneja Ushirikiano wa Kimataifa, Bw. Wilbert Muruke akimsaidia Dkt. Kijazi kuongoza kikao na kuchukua muhtasari.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi, ambaye pia ni Mweyekiti wa sasa wa Umoja wa Taasisi za Hali ya Hewa za nchi za SADC "Meteorological Association of Southern Africa (MASA)", ameongoza kikao cha kwanza cha Bodi ya Umoja huo kwa mwaka 2022 kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 26 Januari, 2022.

Dkt. Kijazi aliongoza majadiliano ya utekelezaji wa Mapango wa Kuhuisha Shughuli za MASA (MASA Rescue Plan) ambapo Bodi iliazimia kuandaliwa kwa mpango kazi (Action Plan) utakaoainisha utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa katika mpango huo.

Aidha, Mwenyekiti Dkt. Kijazi alikitaka kikao hicho kupitia maelekezo ya Kikao cha Mawaziri wa SADC kilifanyika mwezi Julai 2021 yanayohusiana na masuala ya hali ya hewa yaliyoelekezwa kwa MASA.

"Nimeona ni muhimu tukawa na kikao cha kujadili utekelezaji wa maelekezo ya kikao cha Mawaziri wa SADC kilichofanyika mwezi Julai 2021 ili masuala yanayohitaji kufanyiwa kwa haraka yafaniwe utekelezaji". Alizungumza Dkt. Kijazi.

Katika hatua nyingine, Kikao kilifanya uteuzi wa nafasi za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ambapo Lesotho ilipendekezwa kuwa Mwenyekiti mpya na Msumbiji kuwa Makamu Mwenyekiti kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2022 hadi 2024. Mapendekezo hayo yatawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa MASA "MASA Annual General Meeting (AGM)" unaotarajiwa kufanyika mwisho wa mwezi Februari, 2022 kwa ajili ya kupitishwa rasmi.

Lengo la kikao hicho lilikuwa kujadili utekelezaji wa masuala muhimu ya sekta ya hali ya hewa yanayohusiana na majukumu ya MASA. Tanzania kupitia TMA ni Mwenyekiti wa MASA tangu Agosti, 2019 na Lesotho ndiye Makamu Mwenyekiti. Wajumbe wa Bodi ya MASA ni Tanzania, Lesotho, Afrika ya Kusini, Msumbiji na Namibia.

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2022

Kwa ujumla vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi. Kwa upande mwingine, vipindi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini hususan yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache katika kipindi cha mwezi Februari, 2022. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi. |
| Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache katika kipindi cha mwezi Februari, 2022. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza ya mwezi. |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Upungufu wa mvua unatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo linatarajiwa katika maeneo machache hususan wiki ya nne ya mwezi February, 2022. |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Upungufu kidogo wa mvua unatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi February, 2022. |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Februari, 2022. |
| Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Hata hivyo, upungufu kidogo wa mvua unatarajiwa katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2022. |
| Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2022. |
| Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi kwa mwezi wa February, 2022. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu ya mwezi Februari, 2022. |

# KISWAHILI CHETU

## ISTILAHI ZA HALI YA HEWA

### Tuangazie herufi J, K & L:

| | |
|---|---|
| sea breeze | upepo mwanana wa bahari |
| sea level | usawa bahari |
| sea surface | usobahari |
| strong wind | upepo mkali |



upepo mkali




**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa
Kituo Kikuu cha Utabiri

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV

Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
388 Br. Morogoro
S.L.P 3056,
16102 Dar es Salaam, Tanzania.